# USAWA
# UHURU
# URAIA



*AMNESTY INTERNATIONAL KENYA*
*MFUMO WA KIMKAKATI*
*2021-2023*

KENYA

AMNESTY INTERNATIONAL

# TABLE OF CONTENTS


01 UJUMBE WA MWENYEKITI NA MKURUGENZE MTENDAJI

02 MUHTASARI

04 UCHAMBUZI WA SHIDA NA NADHARIA YA MABADILIKO

09 NADHARIA YA MATOKEO YA MABADILIKO

10 NGUVU, UDHAIFU, FURSA NA VITISHO

11 MABADILIKO YA TAASISI NA RASILIMALI ZINAZOHITAJIKA

14 UPANGAJI, UFUATILIAJI, TATHMINI NA KUJIFUNZA

15 TUNAKUHITAJI

16 TIMU YETU

# Ujumbe Wa Mwenyekiti



Tangu uzinduzi wa shirika la Amnesty miaka sitini iliyopita, imekuwa moja ya mashirika makubwa zaidi ya utetezi wa haki za binadamu ulimwenguni. Amnesty International Kenya ni sehemu moja ya vuguvugu hili linalozidi kuwa na ushawishi wa harakati hii ya zaidi ya wafuasi milioni kumi.

Usawa, Uhuru na Uraia labda ni maneno matatu muhimu zaidi kwetu sisi sote leo. Hatuwezi kukuza jamii ambayo ni kioo cha katiba yetu bila ya kila mwanadamu kuelewa na kudai haki na uhuru wake.

Katika kipindi cha miaka mitatu ijayo, bodi yetu ya kitaifa na wafanyikazi wetu watachochea duru za dhamiri zinazoendeleza haki kamili za uraia na Serikali nzuri na inayowajibika. Tunajitolea kufanya kazi na wafuasi wetu, wanachama na washirika katika asasi za kiraia na Serikali. Kwa kufanya hivyo, tutaimarisha maoni ya umma, ushirika na mkutano wa amani na pia kupunguza ubaguzi, ufisadi na kutojitolea.

Haya yote hayata wezekana bila ushirika wako. Tunakualika usome mkakati huu kwa uangalifu, kisha ufuate, ushiriki na ujiunge na kampeni zetu. Tutambulishe kwa familia yako, mahali pako pa kazi, ibada na ujifunzaji. Tualike tufanye kazi na wewe na jamii zako. Tunatarajia kufanya kazi pamoja tukitekeleza mkakati huu.

***Renee Ngamau***
***Mwenyeketi AIK***

# Ujumbe Wa Mkurugenzi Mtendaji




Mkakati huu mpya unasasisha maono yetu kwa Kenya na ulimwengu. Mfumo wa mkakati yetu ya awali, Haki za Kijamii, Haki na Heshima 2018-2020, uliongozwa na Katiba ya 2010. Tulijitolea kutetea makazi ya uma na afya, kuelimisha uma kuhusu haki ya binadamu na haki ya kuishi. Tulijitolea pia kwa tamaduni ya shirika inayoongozwa na wafanyikazi wenye bidii na hodari na wanaosimamiwa na bodi ya kitaifa.

Kwa miaka mitatu iliyopita, tulibadilisha usimamizi na nguvu kutoka kwa bodi ya ushauri ya watu watatu na tukaunda bodi ya kisheria ya Wakenya kumi na moja. Wafanyikazi wetu walikua kutoka wafanyikazi kumi hadi kumi na tano. Tuliimarisha uhusiano na Serikali ya Kenya, Bunge, Mashirika huru na Tume za Katiba pamoja na vyama vya wafanyikazi na vituo vya haki ya kijamii

Sauti yatu ilibaki kuwa ya matumaini, mapendekezo na yenye usawa wakati wa janga la COVID-19. Uanachama wetu umeongezeka mara nne na wanachama wanahusika zaidi katika kampeni zetu. Tumetofautisha msingi wetu wa ufadhili kwa asilimia ishirini na tuna washirika wapya wa ufadhili. Tuliekeza asilimia themanini ya mifumo yetu ya usimamizi katika dijitali. Kuwa Amnesty ni wito na fursa ya kukutumikia.

Tunatarajia kufanya kazi pamoja tukitekeleza mkakati huu.

***Irungu Houghton***
***Mkurugenzi Mtendaji***

# 1.MUHTASARI



*Stephen Mwangi, Andrew 'ZamaZama' Okolla, Anami 'Daudi' Toure ,and Javan The Poet - Wanaume wa Amnesty Waheshimiwa*

**Kenya ina katiba endelezi, lakini kukosekana kwa usawa pamoja na kutokujali na ufisadi kunasababisha kutokuwa na matumaini kwa mamilioni.**

Amnesty International Kenya ilisajiliwa kama shirika lisilo la kiserikali mnamo 2012 baada ya zaidi ya muongo mmoja wa ulinzi wa haki za binadamu kutoka ofisi zetu za London au Kampala. Mfumo wetu wa Mkakati, Haki za Kijamii, Haki na Heshima 2018-2020, ulitangaza dira mpya ya kazi yetu. Ilihamasishwa na Katiba ya 2010, utetezi wa makazi, afya, elimu ya haki za binadamu na lengo la mpango wa haki. Tulikuza utamaduni wa shirika linaloongozwa na wafanyikazi wenye bidii na hodari na wanaosimamiwa na bodi ya kitaifa.

Kati ya 2018-2020, tulibadilisha usimamizi na nguvu kutoka kwa bodi ya ushauri ya watu watatu na kuunda bodi ya sheria ya Wakenya kumi na moja. Idadi ya wafanyikazi ilikua kutoka wafanyikazi kumi hadi kumi na tano. Tuliimarisha uhusiano na Baraza la Mawaziri, Bunge, Wakala Huru na Tume za Katiba pamoja na mashirika ya kiraia, vyama vya wafanyikazi na mashirika ya haki za binadamu ya jamii.

Tulibuni mbinu za kisasa katika utetezi wa haki za binadamu na kudumisha sauti ya kitaifa inayoonyesha pendekezo na usawa

Uanachama umeongezeka mara nne na wanachama na umma wanahusika zaidi katika kampeni zetu. Wafanyikazi wetu wanamtazamo wa mawazo ya nje-ndani ambayo yanayojionyesha katikaulinzi wawatu walio katika hatari na kusababisha mabadiliko makubwa ya sera ya kitaifa na tabia. Tumetofautisha ufadhili wetu kwa asilimia ishirini na tunawashirika wapya wa ufadhili. Tulipanga mikutano ya mtandaoni na kubuni mifumo mpya ya usimamizi wa fedha, rasilimali watu na wanachama tulipokuwa tunafanya kazi manyumbani mwetu wakati huu wa janga la COVID-19.

Mkakati huu umearifiwa na mapendekezo kutoka kwa tathmini yetu huru na ufahamu kutoka kwa wafuasi, wafanyikazi na Bodi katika mwaka wa 2020. Mkakati huu utawezesha:

- Ushirikiano mkubwa na vipaumbele vya mkakati wa Amnesty International (2021 – 2029) zinazozungumzia uhuru wa raia na usawa na uhuru kutokana na ubaguzi,
- Ukuaji wa wanachama na ushiriki mkubwa katika kampeni na utawala wetu,
- Upangaji wa kina wa dijitali na ana kwa ana,
- Ufuatiliaji na tathmini kali,
- Mseto wa kifedha na uthabiti wa shirika kupitia michango ya kifedha ya Wakenya,
- Bodi ya wanaharakati iliyo na mtazamo wa nje,
- Utambuzi wa sehemu tofauti na ushiriki mzuri zaidi na harakati za kimataifa.



*Stephen Mwangi - Mwanaume wa Amnesty Mheshimiwa*

# 2.UCHAMBUZI WA SHIDA NA NADHARIA YA MABADILIKO



*Rachael Mwikali - Mjumbe ya bodi wa Amnesty*

Kenya ni mojawapo ya nchi zilizo na katiba endelezi ulimwenguni. Licha ya hili, tofauti za kisiasa, tofauti za kiuchumi, kutengwa kwa jamii, kutojali na ufisadi husababisha kutokuwa na matumaini kwa mamilioni. Asilimia hamsini na mbili ya Wakenya hawaamini kwamba kuna usawa chini ya sheria. Wakenya wengi wanaamini hatari kubwa kwa maisha yao ni kunyimwa huduma za afya, mauaji haramu ya polisi na unyanyasaji, njaa na vizuizi kwa uhuru wa kujieleza. Wakenya wanaogopa unyama wa polisi zaidi umasikini.

**Haki sio mwisho wa safari au maadili fulani. Ni barabara tunayopaswa kutembea kila siku, tukijua kuna wengine watakaokuja baada yetu tunapochoka.**

Ukosefu wa usawa, ufisadi mkubwa na matumizi mabaya ya ofisi huzuia ahadi ya msingi ya kikatiba, kipengele cha haki za binadamu. Bila mabadiliko, watu watakosa fursa ya kufurahia haki na uhuru wao wa kimsingi. Kenya kamwe haitakuwa jamii iliyo wazi kabisa na ya kidemokrasia iliyojengwa juu ya kanuni za utu wa binadamu, usawa na uhuru (Kifungu cha 18 na 20).

Miaka mitatu iliyopita kumekuwa na mafanikio makubwa yanawafaidi mamilioni ya Wakenya. Bima ya kitaifa ya afya na elimu ya msingi na sekondari kwa ujumla imepanuka na kusababisha kupungua kwa vifo vya akina mama na wanafunzi kuacha shule. Kuongezeka kwa uwekezaji sasa kunafadhili mipango ya makazi ya umati unaokaa katika makazi yasiyo rasmi ambayo muongo mmoja uliopita yalikuwa marufuku kwa wapangaji wa miji.

Kumekuwa na maendeleo katika mageuzi ya haki ya jinai kutokana na uongozo wa Baraza la Kitaifa linaloshughulikia maswala ya Utawala wa Haki. Ijapokuwa kwa mvutano, huduma ya Polisi ya Kitaifa, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma na Mahakama wametumia uhuru wao wakisaidiwa na mashirika ya haki za binadamu. Huduma ya kitaifa ya Magereza imedumisha mageuzi kuelekea mifumo ya ukarabati na sera wazi ya wageni, tathmini ya akili na msaada, fursa za kupata mapato na msongamano mdogo katika magereza.

Watetezi wa ugatuzi wanaweza kujivunia. Nguvu za kisiasa na kifedha zimewafikia kwa kiasi kikubwa vitengo 47 vya serikali ndogo za kaunti kulingana na Kifungu cha 174 cha Katiba. Njia mpya za uangalizi kama vile Bunge la Kaunti, haki ya kupata habari na sheria za ushiriki wa umma na fora za kaunti zimepanua nafasi kwa raia kushawishi utawala wa eneo.





*Javan The Poet - Mwanaume wa Amnesty Mheshimiwa*



Kwa masikitiko, mafanikio makubwa yamechafuliwa na kashfa kubwa za kitaifa za ufisadi, ongezeko la deni la umma na kupungua kwa ukusanyaji wa mapato. Zaidi ya theluthi moja ya Wakenya wanaamini ufisadi na matumizi mabaya ya ofisi ndio shida kuu inayokabili ugatuzi na kunyimwa haki za binadamu. Jaribio la makusudi la kuzuia ushiriki wa umma husababisha ufisadi. Lakushangaza, muongo mmoja baada ya Wakenya kupitisha katiba, chini ya asilimia 8 ya raia wanajua na wanaweza kutetea bajeti za kitaifa au kaunti na mipango ya maendeleo.

Vizuizi vinne kwa sasa vinazuia maono ya Kenya inayoongozwa wazi, ya kidemokrasia na yenye haki. Sera zinazoendeshwa na ununuzi na vichocheo vya uwekezaji mwishowe huaribu mipango mikubwa ya miundombinu ya umma ya Kaunti na kitaifa. Utamaduni wa ulafi upo kati ya maafisa wengi wa usalama ambao huwapora na kuwasaka masikini na waliotengwa.

Tume za kikatiba na tume huru zinazofadhiliwa kwa kiasi kidogo zimekuwa tuzo kwa wanaotii kisiasa. Vyombo vya habari na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanazidi kufadhiliwa kwa kiasi cha chini hivyo kuwa na ufanisi mdogo.

Sauti na uharaka ya Wakenya, wanaoshinikiza dhidi ya ukatili wa polisi, kufukuzwa kwa nguvu, kunyimwa huduma za afya na uharibifu wa mazingira, imetengwa sana. Licha ya nyakati tatu muhimu za ukombozi katika kizazi hiki – vyama vingi (1992), ushindi wa NARC (2002) na katiba ya 2010 – umma unazidi kudhoofika. Matarajio ya utawala mpya mnamo 2022 umedhoofishwa vibaya na dhana iliyoenea kwamba hakuna viongozi waaminifu au wanaojibika. Hata kama wako, wengi wanaamini miundombinu ya usimamizi wa uchaguzi imetekwa na itawazuia kujitokeza kwa hali yoyote.



*Janet Mbugua - Mwanamke wa Amnesty Mheshimiwa*

Ikumbukwe uhamasishaji wa kisiasa wa zamani wa kikabila, chaguo la uwongo kati ya “nasaba” na “masikini” sasa linaenezwa nyuma ya mazungumzo muhimu ya kitaifa yaliyosababishwa na Building Bridges Initiative. Hakuna upande unaonekana kuwa tayari kuacha ubinafai. Vyombo vya habari vimetumiwa kuficha mikakati mpya ya kupambana na ufisadi ambayo inaweza kuhakikisha kuwa miradi mikubwa ya baadaye itawanufaisha watu wote na sio wanabiashara wakibinafsi pekee. Ukizingatia viongozi wachache na taasisi chache zinazoaminika, raia wengi wanapoteza uvumilivu. Viwango vya uaminifu vinazidi kupungua.

Kuwepo kwa viongozi wa kisiasa ambao hutafuta uungwaji mkono kwa kupenda tamaa na chuki, kuongezeka kwa msimamo mkali, matamshi ya chuki, kupuuza na vurugu za serikali huwaacha wengi wakiamini tunaishi katika ulimwengu usiokuwa na haki za binadamu. COVID-19 imesababisha mifumo ya utawala wa udikteta na kuhamasisha utetezi wa haki za binadamu. Kikubwa kati yao ni harakati za ulimwengu za #BlackLivesMatter na harakati za kupinga ubaguzi. Upigaji kura uliomtimua Trump mamlakani mnamo Novemba 2020 hutoa masomo mengi kwa watetezi wa haki za binadamu kote ulimwenguni.

Mwisho wa mwaka 2020, majirani wote wa Kenya wanaonekana kuelekea kwenye mizozo. Kuna mivutano ya Kisiasa na mzozo mkali nchini Ethiopia, chaguzi zenye utata nchini Tanzania na Uganda na kutokuwa na uhakika upya kuhusu mradi wa ujenzi wa serikali nchini Somalia. Kwa kuzingatia utulivu wa Kenya na kuongezeka kwa ushawishi wa kimataifa, Amnesty International Kenya lazima pia iunge mkono ushawishi wa Amnesty na harakati zake za usalama.




*Kevin Mwachiro - Mjumbe wa bodi ya Amnesty*

Ijapokuwa Trump ameondolewa mamlakani, ufuasi wake na siasa za ukiritimba ni ngumu kung'oa Amerika na kwingineko. Tutawapa Wakenya ufahamu, rasilimali na majukwaa ya kushughulikia moja kwa moja ubaguzi wa kitaasisi, vurugu, ufisadi na ukosefu wa uwajibikaji. Kutokana na ushawishi wa Kenya ulimwenguni, tutaimarisha mshikamano wetu na harakati barani Afrika na kwingineko.

Kwa kufanya hivyo, tutarudisha ujasiri wa vizazi vya watetezi wa haki za binadamu ambao kihistoria walitenda kwa msukumo mmoja. Sheria zingine zinahitajika kuvunjika kwa makusudi ili Kenya na ulimwengu upate nafuu. Walijua, kama sisi pia sasa, mbele ya ukosefu wa haki na ubaguzi, jamii zenye mshikamano, zenye huruma na zinazojali zimekuwa zikiundwa na waasi. Kwa kuongezea, wasifu bora zaidi wa kibinafsi hupatikana katika nyakati zilizo na kutokuwa na uhakika na hatari. Tunakubali jukumu hili la kihistoria na tunakualika ujiunge nasi.

Ni wakati ambapo Amnesty International Kenya ibadilishe maono yake, dhamira na ujumbe wa kimkakati. Mapitio yetu huru ya nje yalidhihirisha kwamba tumetimiza ahadi tuliyotoa katika Haki za Mfumo wa Mkakati, Utu na Haki (2018-2020). Tumebadilika sana tangu 2012, hata 2018. Uchambuzi huu wa ulimwengu na kitaifa unahitaji kuendelea kubadilisha utamaduni wetu wa shirika, kuanzia fikra mpya, ujuzi na miundo na kuunda tena dhamira yetu ya kubaki muhimu kitaifa na kimataifa. Tunajitolea kufanya hivi.

**Wakenya, ni bora kufa kwa miguu yako kuliko kuishi kwa magoti**

**CPA Spencer Sankale,**
**Mfichuzi wa Mara Heist**





*Crystal Asige - Mjumbe wa bodi ya Amnesty*

# 3.NADHARIA YA MATOKEO YA MABADILIKO

Amnesty International Kenya inaimani na jamii ambayo kila mwanadamu anaelewa na kudai haki na uhuru wao wa kikatiba. Tupo kuwezesha duru za dhamiri na harakati zinazoweza kuendeleza haki kamili za uraia kwa wote na hali inayofaa na inayowajibika. Pamoja na wafuasi, wanachama na washirika katika asasi za kiraia na serikali, tutaunda utamaduni wa wanaharakati ambao unaimarisha maoni ya umma, ushirika na mkutano wa amani na kupunguza ubaguzi, ufisadi na kutokujali katika viwango vya kitaifa na kaunti.

| **Matokeo Ya Programu** | **Jamii ambayo kila mwandamu anaelewa na kudai haki na uhuru wake wa kikatiba** | |
|---|---|---|
| **Nguzo Mbili** | **Lengo la AI 1:**<br>**Uraia na Uhuru wa Kujieleza**<br>(Nakala: 1)<br>Kuimarisha uhuru wa kujieleza na kushirikiana<br>Kupanua nafasi ya uraia kwa uwajibikaji wa umma | **Lengo la AI 2:**<br>**Ukosefu wa Usawa na Ubaguzi**<br>(Nakala: 26, 27-29, 43)<br>Kupunguza kutokuwa na usawa na ubaguzi unoa tokana na utambulisho<br>Kupunguza athari za ufisadi kwa haki za binadamu |
| **Kampeni Zetu** | Mshikamano na zana kwa watu walionyimwa uhuru wa kujieleza, maisha, ushirika na mkutano<br>Kuratibu vitendo na duru za Amnesty na washirika + kuwezesha jamii / watu walio katika hatari | Mshikamano na zana kwa watu walioathiriwa na afya, kufukuzwa na ubaguzi wa kijinsia / utambulisho na vurugu<br>Kuratibu vitendo na duru za Amnesty na washirika + kuwezesha jamii / watu walio katika hatari |

## Vitengo vitano vya msaada na mtangamano

**Mawasiliano na Uanachama**

Utambulisho wa chapa na mkakati wa mawasiliano ulio na msingi wa matumaini | tovuti, CRM, vyombo vya kijamii na matukio | mahusiano na waandishi wa habari | kuratibu upanuzi wa wanachama na mawasiliano

**Elimu ya Haki za Binadamu**

Kuratibu mtaala na vilabu vya shule na sura za vyuo vikuu | kozi za haki za binadamu mkondoni na nje ya mkondo | Uzalishaji wa vifaa vya wanaharakati | kuhamasisha sauti na uwakala wa vijana

**Uimara wa shirika + MEL**

Ufadhili wa mseto na utekelezaji wa uthabiti wa kifedha | uwekezaji unaotegemea mali | hazina ya haki za binadamu | mwenendo wa uhisani

**Fedha na Utawala**

Mapokezi | ununuzi | kifedha | usimamizi wa shughuli | taarifa ya shirika | ufuatiliaji na tathmini | Ukagu

**Mkurugenzi Mtendaji**

Katibu wa bodi | Uwakilishi wa kiwango cha juu | harambee | utafiti wa sera | rasilimali watu | mshikamano wa kimataifa

# 4.NGUVU, UDHAIFU, FURSA NA VITISHO

## NGUVU

- 85% ya wafuasi wetu wanataka kujitolea zaidi,
- Chapa yetu inaonekana kitaifa na inaaminika na ofisi muhimu za serikali na umma,
- Tumeonyesha uwezo wa ulinzi wa mjibu wa kwanza,
- Bodi ya usimamizi wenye hamu, wepesi na ujasiri na kuheshimiwa kwote katika vuguvugu la Amnesty.

## UDHAIFU

- Uzoefu mdogo wa kampeni za haki za kupambana na ufisadi,
- Mada ya usawa bado ni geni kwetu,
- Mfumo duni wa ufuatiliaji na tathmini.

## FURSA

- 40% ya wafuasi wetu wanataka kuwashirikisha wengine, kuandaa mduara ya Amnesty au kuandaa hafla,
- 84% wanataka tufanye kazi na watu wanaoishi katika umasikini na kutengwa,
- Fedha zetu zina ongezeka na hazina vizuizi.

## VITISHO

- Mapato ya vikundi vya kijamii zinaedele kupuanga,
- Siasa za udhehebu, Habari za uongo na ubaguzi wa kina wa kijamii unaongezeka tuna vyo elekea uchaguzi mkuu wa 2022,
- Viwango vya juu vya Habari za uongo na matamshi ya chuk

# 5.MABADILIKO YA TAASISI NA RASILIMALI ZINAZOHITAJIKA



*Joram Mwinamo - Mweka hazina wa bodi*

**Mbele ya ukosefu wa haki na ubaguzi, jamii zenye kujali na zinazoshikamana zimeundwa kila mara na waasi. Tunakubali jukumu hili la kihistoria na tunakualika ujiunge nasi.**

Muktadha wetu ni moja ya tete, kutokuwa na uhakika na utata unaoendelea kubadilika. Kutafuta haki, usalama na utu ndani ya muktadha huu kunahitaji uongozi kamili, fikra za "nje-ndani", wepesi wa taasisi na mtandao wa kitaifa. Mwanzoni tuliona wafuasi na wanachama kama lengo la ukuaji wa harakati, sasa tunatambua, kwamba ili tufanikiwe, lazima wawe vichocheo katika vitongoji vyao, sehemu za kujifunzia, sehemu za kazi na vyama.

Kufikia 2023, duru hamsini za dhamiri na washirika watakuwa wakilinda kikamilifu haki za binadamu katika kaunti kumi na tano zilizo na umaskini mkubwa, kutengwa na vurugu. Wanachama wetu 5,000 watahusika kikamilifu katika kampeni zetu na angalau wanachama hamsini wakichangia mara kwa mara kwenye hazina yetu ya kitaifa ya Haki za Binadamu kwa duru zetu za dhamiri. Tutakuwa na ushirikiano wa kimkakati na vyama vitatu vikubwa, vyenye msingi wa watu wengi na vyama vya wafanyikazi. Mahusiano haya yataungana karibu na kampeni za siku 180 za muda mfupi.

Tutakuwa na bajeti ya kila mwaka ya Kshs milioni 150. Jalada lililoongezeka na mseto litaundwa na ufadhili wa RAM (40%), Misingi (50%) na utoaji wa mtu binafsi, uwekezaji, mali (10%). Tutakuwa tumeunda mifumo ya usimamizi na mawasiliano ili kutumia na kuongeza thamani kwa wale ambao hutoa wakati wao, ujuzi na rasilimali kwa harakati zetu.

Robo ya kwanza ya mwaka wa kwanza itatumika kujenga timu yetu, kuelekeza ustadi, kutambua washirika, wenzao na niche yetu ya kimkakati katika kampeni tutakazoendesha mwakani 2021. Mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini utaanzishwa.

Simulizi ya haki za binadamu iliyo na matumaini itakuwa mzingi wa mazungumzo ya sera katika vyama vyetu vya kisiasa, ofisi za serikali na umma. Amnesty itajulikana kwa uhuru wake, ulinzi unaotegemea ushahidi na ulinzi wa jamii zinazoathiriwa. Wafanyakazi wote watawajibika kwa uandikishaji wa wanachama. Wafanyikazi katika kampeni zetu tofauti watapewa jukumu la kufanya kazi moja kwa moja na wanachama na duru za dhamiri. Tutakuwa sehemu tendaji ya kitaifa inayofanya kazi ndani ya jamii ya kimataifa ya sehemu za Amnesty. Tutaongoza ushawishi wa kusonga karibu na jamii ili kupanua uwepo wa Amnesty katika Afrika Mashariki. Harakati kubwa zaidi za haki za binadamu nchini na ulimwenguni zitajivunia utendaji wetu na ubunifu.






*Aurelia Miheso - Mfanyikazi wa Amnesty*

# 6.UPANGAJI, UFUATILIAJI, TATHMINI NA KUJIFUNZA




*Wakati wa mshikamano nje ya nyumba ya Yassin Moyo*

Kulingana na miongozo kutoka Sekretarieti ya Kimataifa na mazoea mazuri yanayoibuka, Amnesty International Kenya itaunda mfumo kamili na jumuishi wa MEL ambao utaelekeza upangaji, upimaji na kuripoti hatua za kampeni. Kwa mfumo huu wa kimkakati, athari za haki za binadamu ni pamoja na maswala yote yanayohusiana na ufafanuzi wa matokeo muhimu zaidi yaliyopatikana na pia ushiriki wa washirika, wanachama na wafuasi katika mipango ya haki za binadamu. Ni matarajio yetu kukusanya, kupakia, kushiriki na kutumia mafunzo kutoka kwa kazi yetu ya haki za binadamu ili kuongeza uingiliaji na kuboresha utoaji. Tutachukua faida ya majukwaa ya teknolojia iliyopo ili kuboresha mifumo yetu ya MEL. Hasa, tutakusudia kutumia dijiti kuripoti matokeo muhimu ya kampeni kwa wakati halisi.

**Bora kuwasha mshuma kuliko kulaani giza.**

# TUNAKUHITAJI

Kuna njia nyingi za kushirikiana na Amnesty International Kenya. Kupitia kila mmoja yao, unajiunga na jamii ya watu milioni 8 wanaofanya kampeni ya kumaliza ukiukwaji wa haki za binadamu

## Msaidizi

Tusaidie kwa kueneza yaliyomo kwenye viombo vyetu vya kijamii na kuwa na mazungumzo yenye manufaa makubwa na marafiki na familia yako



*Charles Omote - Mwanachama wa Amnesty*




*Bodi na wafanyikazi na baba wa Yassin Moyo nje ya Nyumba ya Moyo*

## Kujitoleaa

Unatafuta mwingiliano zaidi? Jitolee! Toa wakati wako, nguvu na ujuzi kutusaidia kukua na kufikia wale wanaohitaji msaada wetu.

**WWW.AMNESTY.OR.KE/VOLUNTEER**

## Uanachama

Chukua umiliki wa kazi ya Amnesty kwa kuwa mwanachama. Wanachama hulipa ada ya kila mwaka. Tuna viwango 3 vya ushirika wa kuchagua kutoka marupurupu tofauti. Kwa ksh 200 unaweza kuwa mwanachama wa uhuru, kwa ksh 1000 unaweza kuwa mshiriki wa usawa, na kwa 2000 ksh utakuwa mwanachama wa haki.

Kuwa mwanachama hapa:
**WWW.MEMBERS.AMNESTYKENYA.ORG /REGISTER**



*Rose Tinderet - Mwanachama wa Amnesty*




*Stephen Okwany - Mwanachama wa Amnesty*

# TIMU YETU

## BODI


Renee Ngamau


Joram Mwinamo


Kevin Mwachiro



Crystal Asige



Dr.Myrna Kalsi


Awuor Ayiecho


Catherine Mumma



Dr. Simon Kigondu


Rachael Mwikali

## WAFANYIKAZI



Irungu Houghton


Victor Ndede


Lavender Namdiero



Gregg Mwendwa


Demas Kiprono



Stephen Oyugi


Levi Nyamu



Ramadhan Rajab


Aurelia Miheso


Beverly Wakiaga



Joanne Kobuthi-Kuria



Billy Omondi


James Kimila



Mathias Kinyoda


PhilCollins Omondi


Ignatius Yambasa


Diana Gichengo


Elvis Salano


Amy Ochieng




# WASILIANA NASI

Amnesty International Kenya
@AmnestyKenya
@amnesty_kenya
Amnesty International Kenya

+254 (0)20-4283000
amnesty.kenya@amnesty.or.ke
www.amnestykenya.org
Riverside Studios (Former Netherlands Embassy)
Riverside Lane Off Riverside Drive
Nairobi, Kenya

KENYA AMNESTY INTERNATIONAL